Kuanguka na Kuinuka kwa Patro

Na

Ellis P. Forsman

(The Fall and Rise of Peter)

Kuanguka na Kuinuka kwa Petro

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Kuanguka na Kuinuka kwa Petro

Marko 14:27-72

Mtume Petro ni mwandishi wa Biblia anayependwa na wengi. Alikuwa mvuvi. Wavuvi wengi wamechakaa na wachafu.

Wakati mwingine alikuwa mwenye haraka.

Mat. 26:32-34, "*Lakini baada ya kufufuka kwangu nitawatangulia kwenda Galilaya. Petro akajibu akamwambia, wajapochukizwa wote kwa ajili yako, mimi sitachukizwa kamwe. Yesu akamwambia, amin nakwambia wewe usiku huu kabla ya kuwika jogoo utanikana mara tatu.*"

Watu wengi husema kwamba wanafanana na Petro.

Kristo alimteua Petro amfuate

Andrea, ndugu yake Petro, alimleta Petro kwa Yesu.

Yohana 1:38-42, "*Yesu aligeuka akawaona wakimfuata, akawaambia mnatafuta nini? Wakamwambia Rabi, (maana yake mwalimu), unakaa wapi? Akawaambia njooni nanyi mtaona. Wakaenda wakaona akaapo, wakakaa kwake siku ile. Nayo ilikuwa yapata saa kumi. Andrea nduguye Simoni Petro alikuwa pamoja na wale wawili waliomsikia Yohana na kumfuata Yesu. Huyo akamwona kwanza Simoni, ndugu yake mwenyewe, akamwambia tumemwona Masihi, maana yake Kristo). akampeleka kwa Yesu, naye Yesu aakamtazama, akasema wewe u Simoni mwana wa Yohana; nawe utaitwa Kefa (tafsiri yake Petro, au jiwe).*"

Alikuwa ni mshirika wa ndani (aliyependelewa na Yesu).

Marko 5:37, "*Wala hakumruhusu mtu afuatane naye, ila Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye Yakobo.*"

Petro alikuwa kiongozi miongoni mwa mitume.

- Marko 1:29, "*Na mara walipotoka katika sinagogi, walifika nyumbani kwa Simoni na Andrea, pamoja na Yakobo na Yohana.*"

- Marko 8:29, "*Naye akawauliza, na ninyi mnasema kuwa mimi ni nani? Petro akamjibu akamwambia, wewe ndiwe Kristo.*"
- Yohana 6:67, "*Basi Yesu akwaambia wale Thenashara, je! Ninyi nanyi mwataka kuondoka?*"
- Mat. 19:27, "*Ndipo Petro akajibu akamwambia, tazama, sisi tumeacha vyote tukakufuata; tutapata nini bassi?*"

Alikuwa wa kwanza kumkiri Kristo.

Mat. 16:13-18, "*Basi Yesu akaenda pande za Kaisaria – Filipi, akawauliza wanafunzi wake akasema, watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani? Wakasema, wengine hunena u Yohana mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yeremia au mmojawapo wa manabii. Akawaambia, nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani? Simoni Petro akajibu akasema, wewe ndiwe Kristo Mwana wa Mungu aliye hai. Yesu akajibu akamwambia, heri wewe Simoni Baryona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni. Nami nakuambia wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.*"

Alihubiri siku ya Pentekoste, na alikuwa mtu imara katika kitabu chote cha Matendo ya Mitume.

- Mdo. 2:1-14, "*Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwapo wote mahali pamoja. Kukaja ghafla toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingi, kama Roho alivyowalia kutamka. Na walikuwako Yerusalemu Wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu. Basi sauti hii iliposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe. Wakashangaa wote, wakistaajabu wakiambiana, tazama hawa wote wasemao si Wagalilaya? Imekuaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo? Warparthi na Wamedi na Waelami, nao wakaao Mesopotamia, Uyahudi na Kapadokia, Ponto na Asia, Frigia na Pamfilia, Misri na pande za Libia kaaribu na Kirene, na wageni watokao Rumi, Wayahudi na waongofu, Wakrete na Waarabu; tunawasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu. Wakashangaa wote wakaingiwa na shaka, wakiambiana maana yake nini mambo haya? wengine walidhihaki wakisema wamelewa kwa mvinyo mpya. Lakini Petro akasimama na wale kumi na mmoja, akapaza sauti yake akawaambia enyi watu wa Uyahudi, na ninyi nyote mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu.*"

- Mdo. 2:37-41, "*Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, tutendeje ndugu zetu? Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya, akisema, jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi. Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.*"

Mtume huyu mkubwa, hataivyo, alikuwa na matatizo yake. Alianguka kwa nyakati hata nyakati.

Katika somo hili, tunataka kuangalia baadhi ya vitu vilivyochangia anguko la Petro na kuinuka kwake.

Petro alikuwa na ujasiri ndani yake

Hii inaonekana kwa maneno yake.

Marko 14: 27-29, "*Yesu akawaambia mtakunguwazwa ninyi nyote kwa ajili yangu usiku huu; kwa kuwa imeandikwa, nitampiga mchungaji na kondoo watatawanyika. Lakini baada ya kufufuka kwangu, nitawatangulia kwenda Galilaya. Petro akamwambia, hata wajapokunguwazwa wote, lakini siyo mimi.*"

Ni upumbavu kwa mwanadamu kuamini moyo wake mwenyewe.

Mit. 28:26, "*Mwenye kujitumaini moyo wake ni mjinga; bali yeye aendaye kwa busara ataokolewa.*"

Mtu yeyote anawezaa kuanguka.

Mtume Paulo alitaambua ukweli huu.

1 Kor. 10:12, "*Kwa hiyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke.*"

Lazima kila mara tuwe macho.

Hivyo basi, ujasiri binafsi ulikuwa ni hatua katika anguko la Petro.

Petro alifanya ahadi ya haraka au matendo

- Mat. 17:1-5, "*Na baada ya siku sita Yesu akawatwaa Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye, akawaleta juu yam lima mrefu faraghani; akageuka sura yake mbele yaao; uso wake ukang'aa kama jua, mavazi yake yakawa meupe kama nuru. Na tazama wakatokewa na Musa na Eliya, wakizungumzaa naye. Petro akajibu akamwambia Yesu, Bwana ni vizuri sisi kuwapo hapa, ukitaka nitafanya hapa vibanda vitatu, kimoja chako*

wewe, na kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya. Alipokuwa katika kusema, tazama wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama sauti ikatoka katika lile wingu, ikisema Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu ninaye pendezwa naye; msikieni yeye."

- Marko 14:31, "*Naye akazidi sana kusema, ijaponipasa kufa nawe, hata hivyo sitakukana kamwe. Na wote wakasema vilevile.*"

Petro alichukua maamzi pasipo kufikiria.

Alishindwa kuhesabu gharama kwa kauli kama hiyo.

Yohana 13:36-38, "*Simoni Petro akamwambia Bwana unakwendapi? Yesu akamjibu, niendako huwezi kunifuata sasa; lakini utanifuata baadaye. Petro akamwambia Bwana kwa nini mimi nisiweze kukufuata sasa? Mimi nitautoa uhai wangu kwa ajili yako. Yesu akamjibu, Je! Wewe utautoa uhai wako kwa ajili yangu? Amin, amin, nakwambia jimbi hawawiki hata weweutakapokuwa umenikana mara tatu.*"

Yesu alisema ni lazima tuhesabu gharama.

- Mat. 16:24, "*Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, mtu yeyote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake anifuate.*
- Luka 9: 57- 62, "*Nao walipokuwa wakienda njiani mtu mmoja alimwambia, nitakufuata kokote utakakokwenda. Yesu akamwambia, Mbweha wana pango, na ndege wa angani wana viota, lakini Mwana wa Adamu hana pa kujilaza kichwa chake. Akamwambia mwingine, nifuate. Akasema , Bwana nipe ruhusa kwanza niende nikamzike baba yangu. Akamwambia waache wafu wawazike wafu wao; bali wewe enenda ukautangaze ufalme wa Mungu. Mtu mwingine pia akamwambia Bwana nitakufuata lakini nipe ruhusa kwanzaa nikawaaage watu wa nyumbani mwangu. Yesu akamwambia mtu aliyetia mkono wake kulima, kisha akaangalia nyuma, hafai kwa ufalme wa Mungu.*"

Baada ya kauli ya Petro yenye msisitizo na ya haraka ambayo haiwezi kumkana Kristo, Yesu alisema angeweza.

Marko 14:30, "*Yesu akamwambia, amin nakwambia wewe leo usiku huu, kabla ya kuwika jogoo mara mbili, utanikana mara tatu.*"

Petro alikana hata zaidi.

Marko 14:31, "*Naye akazidi sana kusema, ijaponipasa kufa nawe, hata hivyo sitakukana kamwe. Na wote wakasema vilevile.*"

Petro aliacha ulinzi wake akalaa.

Marko 14:32-38, "*Kisha wakaja mpaka bustani iitwayo Gethsemane; akawaambia wanafunzi wake, ketini hapa mudaa niombapo. Akamtwaa Petro na Yakobo na Yohana pamoja naye,*

akaanza kufadhaika sana na kuhangaika. Akawaambia Roho yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa; kaeni hapa mkeshe. Akaendelea mbele kidogo akaanguka kifudifudi, akiomba ya kuwa ikiwezekana saa hiyo imwepuke. Akasema, Aba, Baba yote yawekana kwako; uniondolee kikombe hiki; walakini si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe. Akaja akawakuta wamelala usingizi, akawaambia Petro, Je! Simony, umelala? Hukuweza kukesha saa moja? Kesheni mwombe, msije mkaingia majaribuni, roho I radhi, laakini mwili ni dhaifu."

Labda ujarisi wake ulimleta katika hatua hii.

Petro alichukua hatua za haraka.

- Yohana 18:1-11, "*Alipokwisha kusema hayo Yesu alitoka pamoja na wanafunzi wake kwenda ng'ambo ya kijito Kedroni, palipokuwapo bustani, akaingia yeye na wanafunzi wake. Naye Yudaa yule aliyetaka kumsaliti, alipajua mahali pale; kwa sababu Yesu alikuwa akienda huko mara nyingi pamoja na wanafunzi wake. Basi Yudaa akiisha kupokea kikosi cha askari na watumishi waliotoka kwa wakuu wa makuhani na Mafarisayo, akaenda huko na taa ya mienge na silaha. Basi, Yesu hali akijua yote yatakayompata, akatokea akawaambia ni nani mnayemtafuta? Wao wakamjibu ni Yesu Mnazareti. Yesu akawaambia ni mimi. Yuda naye aliyemsaliti alikuwa amesimama pamoja nao. Basi alipowaambia ni mimi, walirudi nyuma wakaanguka chini. Basi akawauliza tena, mnamtafuta nani? Wakasema Yesu Mnazareti. Yesu akajibu nimekwisha kuwaambia ni mimi; basi ikiwa mnanitafuta mimi, waacheni hawa waende zao. Ili litimizwe lile neno alilolisema, wale ulionipa sikumpoteza hataa mmoja wao. Basi Saimoni Petro alikuwa na upanga, akaufuta akampiga mtumwa wa Kuhani Mkuu, akamkaata sikio la kuume. Na yule mtumwa jina lake ni Malko. Basi Yessu akamwambia Petro, rudisha upanga alani mwake; je! Kikombe alichonipa Baba, mimi nisikinywee?*"
- Luka 22: 50-54, "*Mmoja wao akampiga mtumwa wa Kuhani Mkuu, akamkata sikio la kuume. Yesu akajibu akasema, Mwe radhi kwa hili. Akamgusa sikio akamponya. Yesu akawaambia wakuu wa makuhani, na maakida wa hekalu, na wazee waliokuja juu yake, Je! Mmekuja wenye panga na marungu kama kukamata mnyang'anyi? Kila siku nilipokuwa pamoja nanyi hekaluni hamkuninyooshea mikono lakini hii ndiyo saa yenu, na mamlaka ya giza. Wakamkamata, wakamchukua wakaenda naye nyumbani kwa Kuhani Mkuu. Na Petro alimfuata kwa mbali.*"

Petro alimkana Bwana wake

Kama tulivyoona, Petro alifuatilia kwa mbali. Haikuwa umarufu kuwa na Yesu kwa wakati huu. Petro ameanza kuonyesha dalili za uoga.

Petro alikaa na watumishi na akajionya kwenye moto. Alikuwa anajaribu kufanya haraka na asijulikane. Alirudi nyuma kwa ajili ya Kristo kwa kambi ya maadui.

Luka 22:55-56, "*Na walipokwisha washa moto katikati ya kiwanja, waliketi pamoja, naye Petro akaketi kati yao. Ndipo mjakazi mmoja aakamwona ameketi mwangani, akamkazia macho akasema, na huyu alikuwa pamoja naye.*"

Petro anaanza kulaani

Sasa amefikia mwisho

Marko 14:67-72, "*Akamwona Petro akikota moto; akamkazia macho, akasema wewe nawe ulikuwapo pamoja na yule Mnazareti, Yesu. Akakana akasema, sijui wala sisikii unayoyasema wewe. Akatoka nje hata ukimbini; jogoo akawika. Na yule kijakazi akamwona tena, akaanza tena kuwaambia waliosimama pale, huyu ni mmoja wao. Akakana tena. Kitambo kidogo tena wale waliosimama pale wakamwambia Petro, hakika u mmoja wao, kwa sababu u Mgalilaya wewe. Akaanza kulaani na kuapiza, simjui mtu huyu mnayemnena. Na mara jogoo akawika mara ya pili. Petro akalikumbuka lile neno aliloambiwa na Yesu, kabla ya kuwika jogoo mara mbili, utanikana mara tatu. Na alipolifikiri, akalia.*"

Huko nyuma alisema, "*Hata kama wote wataudhiwa, siyo mimi.*" Anafanya kinyume.

Kuinuka kwa Petro

Alikumbuka maneno ya Bwana.

Marko 14:72, "*Na mara jogoo akawika mara ya pili. Petro akalikumbuka lile neno aliloambiwa na Yesu, kabla ya kuwika jogoo mara mbili, utanikana mara tatu. Na alipolifikiri, akalia.*"

Alihuzunika kwa matendo yake. Hakufanya kama Yuda, aliyetoka nje na kubadilika.

Petro alichomwa moyo. Alitubu. Alikuwa njiani kurudi. Tukio hilo lilikuwa muhimu katika akili yake katika miaka yake ya mwisho.

1 Pet. 5:6, "*Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake;*"

Hitimisho

Hatua za Petro zinaweza kufuatwa leo.

Sisi pia tunaweza kuanguka.

- Gal. 5:4, "*Mmetengwa na Kristo ninyi mtakao kuhesabiwa haki kwa sheria; mmeanguka na kutoka katika hali ya neema.*"

- 2 Pet. 2:20-21, "*Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza. Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki, kuliko kujua kisha kuiacha ile amri takatifu waliyopewa.*"

Hatupaswi kuwa na ujasiri kupita kiasi. Hatupaswi kufanya ahadi zaa haraka au kauli za haraka. Hatupaswi kuachaa ulinzi wetu, kama baada Petro anavyoagiza.

1 Pet. 5:8, "*Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze.*"

Hatupaswi kumkana Kristo.

Mat. 10:32-33, "*Basi kila mtu atakayenikiri mbela ya watu, nami nitamkiri mbele ya Baba yangu aliye mbinguni. Bali mtu yeyote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni.*"

Kama tumeanguka, nasi tunaweza kuanguka.

- 1 Pet. 2:1, "*Basi wekeni mbali uovu wote na hila yote, na unafiki na husuda na masingizio yote.*"
- Ufu. 2:5, "*Basi kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza. Lakini usipofanya hivyo naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu.*"

Je umekuwa Kristo? Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb.11:6*, "Maana pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana yeye ajye kwa Mungu lazima aamini kwamba yeye ndiye, na kwamba huwapa dhawabu wale wote wamtafutao."* Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17) kijana mmoja jirani yangu miaka sawa na ya kwangu aliniambia kuwa aamini katika Mungu. Kwa vile nilikuwa nimebatizwa, nikachukua muda wa kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ilikuwa nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamab kuna Mungu. Lakini ilikuwa sehemu yenye usalama, niheri aende kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) katika siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda Mungu atamuruhusu aingie mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.
- **Toba.** Matend. 2:38*, "Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*

Matend 11:18, "… *Mungu amewajalia hata mataifa nao toba <u>iletayo uzima."</u>* Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba nyingine, ukafikiria mwenyewe, "kuna mwizi humu ndani!" Na unachukua simu yako na kuwa pigia polisi, ukiwambia kuwa kuna mwizi nyumbani

kwako. Muda mfupi unasikia wanafika na kumshika mwizi. Anapiga kelele, “samahani; samahani!” Anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi lazima aombe msaha kwamba hataiba tena na kubadilisha maisha yake. Ni badiliko la nia linalo leteleza badiliko la matendo. Hicho ndicho tunachotakiwa kufanya kabla hatujawa Wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10*, “Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.”* Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

Kumbuka kwamba kifungu hicho kwamba imani (kuamini), kutubu, na kukiri ni “**KATIKA**” haki, uzima au wokovu. “Katika” inamaanisha kuelekea kitu Fulani; siyo kwamba tayari amesha pata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa ili kuitimiza haki yote, “*Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa. Kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akambatiza. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye.”* (Math. 3:14-17).

Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo zuri kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema “imekuwa kwetu **sisi** “*kuitimiza haki yote*” Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, siyo kwa sababu ni haki yetu.

Hakika, tusipobatizwa, bado tungali katika dhambi zetu. *“Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu*.” (Matend. 2:38). Petro, umesema ni nini maana ya ubatizo? “kwa ajili ya ondoleo la dhambi.” Kwa nini yeyote anaweza kuacha hatua inayotuondoa dhambi?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tuzikwe. “*Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.”* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Paulo (kabla hajaitwa Paulo) kitu kile kile *“Sasa unakaawilia nini? Simama, na ubatizwe ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana.”* (Matend. 22:16).

Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. *"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru 6:4). Utu wetu wa kale lazima ufe. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena.*" (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani yake Mungu kwa kupaka damu yake Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tuko huru na dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuziki mwili kaburini kwa kuweka udongo mdogo juu yake; tunazika mwili.

Kama hujawa Mkristo, kwa nini usizingatie leo?